

Karatasi ya Maelezo

Siku ya Choo Duniani 2022: Kufanya yasiyoonekana kuonekana



Siku ya Choo Duniani 2022 ni lini?

Novemba 19, 2022.

Siku ya Choo Duniani ni nini?

Siku ya Choo Duniani imekuwa Maadhimisho ya kila mwaka ya Umoja wa Mataifa tangu mwaka 2013. Iliadhimishwa mara ya kwanza mnamo mwaka 2001 na Shirika la Vyoo Duniani: www.worldtoilet.org

Lengo la Siku ya Choo Duniani ni nini?

Siku ya Choo Duniani huadhimisha vyoo na kutoa uhamasisho kuhusu watu bilioni 3.6 wanaoishi bila kuwa na usafi unaosimamiwa vizuri. Inahusu kuchukua hatua ya kukabiliana na mgogoro wa usafi duniani na kufikia Lengo la 6 la Maendeleo Endelevu: maji na usafi kwa wote ifikapo mwaka 2030.

Ni nani anayeandaa Siku ya Choo Duniani?

Kila mwaka, Shirika la Maji la Umoja wa Mataifa (UN-Water), ambalo ni utaratibu wa kupanga maji na usafi wa Umoja wa Mataifa, huweka mada kwa ajili ya Siku ya Choo Duniani. Mwaka 2022, mada ni 'maji ardhini na usafi'. Mada zilizotangulia zinaweza kupatikana hapa: www.worldtoiletday.info/archives-2022

Ni nini kinatokea kwenye Siku ya Choo Duniani?

Kabla ya siku hiyo, UN-Water huzindua kampeni ya kimataifa kwenye www.worldtoiletday.org na kwenye mitandao ya kijamii kwa kutumia alama ya reli #WorldToiletDay. Watu binafsi, mashirika, serikali, makampuni, shule na watendaji wengine wengi huiunga mkono siku hiyo kwa kutumia ujumbe rasmi na mali au kwa kuandaa shughuli zao wenyewe za Siku ya Choo Duniani.

Je, ni nini mada ya Siku ya Choo Duniani Mwaka 2022?

Mada ya Siku ya Choo Duniani Mwaka 2022 ni 'maji ardhini na usafi'.

Kampeni ya Siku ya Choo Duniani Mwaka 2022 inahusu nini?

Kichwa cha kampeni ya Siku ya Choo Duniani Mwaka 2022 ni 'Kufanya yasiyoonekana kuonekana'. Tafadhali tumia na urekebishe masimulizi yafuatayo unapozungumzia Siku ya Choo Duniani Mwaka 2022:

Kufanya yasiyoonekana kuonekana

Tunakabiliwa na mgogoro wa usafi duniani. Leo, watu bilioni 3.6 bado wanaishi na vyoo duni ambavyo vinaharibu afya zao na kuchafua mazingira yao. Kila siku, zaidi watoto 800 hufa kutokana na kuhara kunakohusishwa na maji yasiyo salama, usafi na usafi duni wa mwili.

Mwaka huu, Siku ya Choo Duniani inaangazia athari za mgogoro wa usafi kwenye maji ardhini.

Mifumo isiyotosheleza ya usafi hueneza uchafu wa binadamu katika mito, maziwa na udongo na kuchafua rasilimali za maji yaliyo chini ardhini. Hata hivyo, tatizo hili ni kama halionekani. Halionekani kwa sababu hutokea chini ya ardhi. Halionekani kwa sababu linatokea katika jumuiya maskini zaidi na zilizotengwa zaidi.

maji ardhini ni chanzo kikubwa zaidi cha maji safi kwetu. Yanasaidia ugavi wetu wa maji ya kunywa, mifumo ya usafi, kilimo, viwanda na mifumo ya ikolojia. Kadiri mabadiliko ya tabia-nchi yanavyozidi kuwa mabaya na idadi ya watu kungezeka, maji ardhini ni muhimu kwa uhai wetu.

Usafi unaosimamiwa vizuri hulinda maji ardhini dhidi ya uchafuzi wa taka za binadamu. Lengo la 6.2 la Maendeleo Endelevu ni ahadi ya dunia ya kuhakikisha vyoo salama kwa wote ifikapo mwaka 2030. Hii inamaanisha kwamba kila mtu awe na ufikiaji wa choo kilichounganishwa na mfumo wa usafi ambao huondoa na kusafisha taka za binadamu. Lakini sisi tuko mbali sana na lengo hili.

Lazima tufanye kazi kwa wastani wa kasi ya mara nne zaidi ili kuhakikisha kila mtu ana choo salama ifikapo mwaka 2030. Uhusiano kati ya usafi na maji ardhini hauwezi kupuuzwa. Muda unakwisha. Lazima tufanye yasiyoonekana kuonekana.

Ujumbe muhimu ni upi?

1. **Usafi hulinda maji ardhi.** Vyoo ambavyo vimewekwa mahali panapofaa na kuunganishwa kwenye mifumo ya usafi inayosimamiwa kwa usalama, hukusanya, kusafisha na kuondoa taka za binadamu na kusaidia kuzuia taka za binadamu zisiennee na kuingia kwenye maji ardhi.
2. **Usafi lazima uhimili mabadiliko ya tabia-nchi.** Vyoo na mifumo ya usafi lazima ijengwe au kurekebishwa ili kukabiliana na matukio mabaya sana ya hali ya hewa, ili huduma zifanye kazi kila wakati na maji ardhi yalindwe.
3. **Hatua ya usafi inahitajika haraka.** Tuko mbali sana na lengo la kuhakikisha vyoo salama kwa wote ifikapo mwaka 2030. Ikiwa imesalia miaka minane tu, dunia inahitaji kufanya kazi kwa kasi ya mara nne zaidi ili kutimiza ahadi yetu.

Je, mgogoro wa usafi duniani ni nini?

Karibu nusu ya idadi ya watu duniani bado wanaishi bila "choo salama". Kwa ufupi, maana ya "choo salama" ni mfumo wa usafi unaosimamiwa kwa njia salama, kumaanisha choo ambacho hakitumiwi na wanafamilia wa nyumba nyingine, ambacho kinatunza au kuondoa taka za binadamu kwenye eneo, kuzihifadhi salama ili zimwagwe na kutunziwa mahali pengine au kinaunganishwa na mtambo unaofanya kazi wa kusafisha maji machafu.

Watu wanaoishi bila ufikiaji wa mifumo ya usafi inayosimamiwa kwa usalama hutumia vyoo vinavyotumiwa kwa pamoja au vile ambavyo haviondoi kwa usalama taka za binadamu. Karibu watu milioni 500 wanajisaidia nje ('kwenda choo peupe') na watu bilioni 3.6, karibu nusu ya idadi ya watu ulimwenguni, hawajaunganishwa na mifumo ya usafi iliyosimamiwa kwa usalama na hivyo kuacha taka za binadamu bila kusafishwa na kuchafua jumuiya na maji yanayotumika kwa ajili ya kunywa, usafi wa mwili, burudani na uzalishaji wa chakula.

Maeneo ya mijini na vijijini yanakabiliwa na changamoto tofauti. Katika mitaa ya mjini yenye watu wengi, vyoo vya shimo na matanki ya maji machafu yanayopatikana karibu na vianzo vya maji ambavyo huteka maji kwenye dimbwi la maji mafupi husababisha hatari kubwa ya kiafya. Katika mazingira ya vijijini, hasa kwa sababu ya kuwepo kwa nafasi kubwa, ni rahisi kuweka vyoo vya shimo na matanki ya maji machafu mbali na vyanzo vya maji.

Mgogoro huu una athari kubwa kwa afya ya umma, upataji wa elimu, uzalishaji wa kiuchumi na uadilifu wa mazingira. Hasa kwa wanawake na wasichana, udhalilishaji, usumbufu na hatari ya kutoweza kufikia usafi unaosimamiwa kwa usalama ni kikwazo kwa ushiriki wao kamili katika jamii.

Maji ardhini ni nini?

Maji ardhini hupatikana chini ya ardhi katika mapango ya maji, ambayo ni miamba ya kijiolojia, mchanga na changarawe ambayo huhifadhi maji. Maji ardhini ndicho chanzo kikubwa zaidi cha maji safi duniani, yakitegemeza mifumo ya maji ya kunywa na usafi, uzalishaji wa chakula, taratibu za kiviwanda na utendaji mzuri wa mifumo ya ikolojia. Katika maeneo mengi, mapango ya maji yako karibu na uso wa nchi, hivyo kuyafanya yawe hatarini hasa kutokana na uchafuzi wa binadamu kutokana na udongo na maji ya uso wa nchi yaliyo juu.

Je, usafi duni unaathiri jinsi gani maji ardhini?

Kutumia maji ardhini kwa ajili ya kunywa huhatarishwa na utupaji usiodhibitiwa wa kinyesi cha binadamu, hasa katika makazi ya mijini yenye watu wengi na kukosekana kwa mifumo endelevu ya usafi katika miji inayokua kwa kasi na mitaa ya pembeni mwa miji. Haya ni maeneo matano yanayoleta wasiwasi:

1. **Vyoo vya shimo na matanki ya maji machafu:** Katika jumuiya yenye watu wengi, vyoo vya shimo pamoja na matanki ya maji machafu yaliyojengwa na kusimamiwa vibaya yanaweza kusababisha uchafuzi mkubwa wa mapango ya maji ya kina kifupi na vyanzo vingine vya maji vilivyo karibu. Hali hii inaweza kusababisha milipuko ya magonjwa kupitia sehemu za maji zilizochafuliwa na virutubishi vingi kupita kiasi vinavyodhuru katika vyanzo vya maji na maziwa yaliyo karibu.
2. **Kutupa kinyesi kwenye majalala ya ardhi:** Mahali ambapo taka za binadamu zinapelekwa kutoka kwenye vyoo vya shimo na matanki ya maji machafu na kutupwa pamoja na taka nyinginezo katika vituo vya majalala visivyo na safu zisizoweza kupenya maji na bila usimamizi mzuri wa taka, uwezekano wa uchafuzi wa maji ya chini ya ardhi ni mkubwa.
3. **Umwagiliaji wa maji kwa kutumia maji machafu yasiyosafishwa:** Mashamba na mamlaka za manispaa wakati mwingine hutumia maji machafu yasiyosafishwa kufanya umwagiliaji. Hii inaleta hatari kubwa ya afya kwa wakulima na watumiaji wa mboga za majani zinazomwagiliwa maji haya machafu ambayo hayajasafishwa na vilevile yanapofanyiwa karibu na visima vya maji vya umma na makazi ya binadamu.
4. **Kumwagika kwa maji machafu:** Katika miji na majiji ambapo mifereji ya maji machafu hutumiwa kuondoa taka, mipango ya uondoaji wa maji machafu na kutumiwa upya mara nyingi haitoshi, kukiwa na hatari kubwa za uchafuzi wa mapango ya maji yaliyo chini ya ardhi au mito ambapo maji taka yametupwa.
5. **Athari za mabadiliko ya tabia-nchi:** Katika maeneo yenye mvua zinazozidi kuongezeka, vyoo vya shimo, matanki ya maji machafu na mifereji iliyo wazi ya maji machafu yanaweza kufurika, yakieneza taka za binadamu ndani ya udongo na maji ya kwenye uso wa nchi. Kinyume chake, katika maeneo yenye ukame unaozidi kuwa mbaya, mifumo ya usafi kama vile vyoo vya kumwaga maji inaweza kuwa isiyoweza kutumika, hali inayowalazimisha watu wajisaidie nje.

Je, huduma za usafi hulinda vipi maji ardhi?

Usafi unaosimamiwa vizuri na kuwekwa mahali panapofaa huwalinda binadamu na maji ardhi dhidi ya vimelea kwenye taka za kinyesi. Mfumo salama na endelevu wa usafi huanza na choo ambacho kinachukua taka za binadamu kwa ufanisi katika mazingira salama, yanayofikika na yenye hadhi. Ama, taka hizo kisha huhifadhiwa katika tanki, ambazo zinaweza kusafishiwa kwenye sehemu hiyo ambapo taka oevu inapenya kwenye udongo na mango inaweza kumwagwa baadaye na huduma ya ukusanyaji. Au inasafirishwa na mfereji wa maji machafu uliunganishwa na mtambo wa kusafisha kisha kutupwa kwa usalama au kutumiwa upya. Matumizi mapya salama ya taka za binadamu zilizosafishwa yanaweza kukamata uzalishaji wa hewa ya ukaa ili kutumiwa kwenye uzalishaji wa nishati na kukipa kilimo chanzo cha kuaminika cha maji na virutubisho.

Mifumo endelevu ya usafi inahitaji kuweza kuhimili mafuriko ya mara kwa mara, ukame, mabadiliko katika upatikanaji wa maji na kupanda kwa usawa wa bahari kunakosababishwa na mabadiliko ya tabia-nchi, ili huduma ziweze kufanya kazi kila wakati na maji ardhi yalindwe. Katika maeneo yanayokabiliwa na uhaba wa maji na kupungua kwa upatikanaji wa maji ardhi, maji machafu yaliyosafishwa yanaweza kutumika kuongeza maji kwenye hifadhi za chini ya ardhi na kujaza tena maji ardhi.

Maeneo ya kulinda maji ardhi ni muhimu, kama sehemu ya njia maalumu na jumuiishi ya kuhakikisha mifumo ya usafi, mipango ya matumizi ya ardhi na utekaji wa maji haiathiri vibaya ubora na wingi wa rasilimali za maji ardhi, hasa katika maeneo ambayo hifadhi za maji ardhi zipo karibu na uso wa nchi.

Kwa nini tunapaswa kujali kuhusu uchafuzi wa maji ardhi?

Kurekebisha uchafuzi wa maji ardhi unaosababishwa na binadamu mara nyingi ni mchakato mrefu na mgumu. Hii huongeza gharama za usindikaji wa maji ardhi na wakati mwingine hata huzuia matumizi yake. Kuchunguza, kulinda na kudumisha kwa kutumia maji ardhi kwa uendelevu kutakuwa muhimu ili kuishi na kuzoea mabadiliko ya tabia-nchi na kukidhi mahitaji ya idadi ya watu inayoongezeka.

Kwa nini kutatua mgogoro wa usafi ni muhimu?

Kuweza kufikia huduma za usafi zinazosimamiwa kwa usalama, pamoja na huduma za maji ya kunywa zinazosimamiwa kwa usalama na vifaa na tabia nzuri za usafi wa mwili, ndio msingi wa afya ya umma na kwa hivyo ni muhimu kwa upataji wa haki nyingine zote za binadamu. Vyoo huchochea uboreshaji wa afya, usawa wa kijinsia, elimu, uchumi na mazingira. Hasa kwa wanawake na wasichana, vyoo nyumbani, shuleni na kazini huwasaidia kutimiza uwezo wao na kutekeleza jukumu lao kamili katika jamii, hasa wakati wa hedhi na ujauzito.

Wafanya maamuzi wanaweza kufanya nini kuhusu usafi na uhusiano wake na maji ardhini?

Uhusiano kati ya maji ardhini na usafi daima umekuwa muhimu sana lakini hautambuliwi kikamilifu. Lazima tulinde maji ardhini dhidi ya uchafuzi na tuyatumie kwa uendeleu, tukisawazisha mahitaji ya watu na sayari.

Jukumu muhimu la maji ardhini katika mifumo ya maji na usafi lazima lionekane katika utungaji wa sera. Zaidi ya hayo, chini ya SDG 6 Global Acceleration Framework (Mfumo wa Kuharakisha wa Kimataifa wa SDG 6), hasa katika maeneo ya utawala, kujenga uwezo, takwimu na habari, uhusiano kati ya maji ardhini na usafi unahitaji kuimarishwa kupitia sera jumuishi na utekelezaji wake unaoratibiwa. Ili kufanikisha hilo, wataalamu wa maji ardhini na usafi, watunga sera na watendaji lazima wote waongeze ushirikiano wao.

Hatua juu ya usafi, kwa nini ni ya haraka?

Lengo la 6 la Maendeleo Endelevu ni kuhakikisha upatikanaji na usimamizi endelevu wa maji na usafi kwa wote ifikapo mwaka 2030.

Lengo la 6.2 la SDG ni "kufanikisha upatikanaji wa usafi na usafi wa mwili wa kutosha na wa usawa kwa wote na kukomesha kwenda choo peupe, kwa kuzingatia mahitaji ya wanawake na wasichana na wale walio katika hali ngumu."

Kwa sasa, dunia imepungukiwa sana katika kutimiza SDG 6.2. Leo, watu bilioni 3.6 bado wanaishi bila huduma za usafi zinazosimamiwa kwa usalama.

Takwimu za hivi karibuni zinaonyesha kwamba, kwa wastani, serikali lazima zifanye kazi kwa kasi ya mara nne zaidi ili kutimiza ahadi ya SDG 6.2 ndani ya miaka minane ijayo. UN-Water inauhimiza ulimwengu uchukue hatua kupitia SDG 6 Global Acceleration Framework na viharakishaji mahususi kwa ajili ya usafi vilivyowekwa katika ripoti ya *Hali ya Usafi Ulimwenguni*.

Kampeni ya Siku ya Choo Duniani Mwaka 2022 inawataka wafanya maamuzi na watunga sera waharakishe kasi ya maendeleo kuhusu usafi na kuhakikisha uhusiano kati ya usafi na maji ardhini unaonekana katika sheria na miongozo inayohusiana katika ngazi zote za kiutawala, kuanzia kimataifa, kitaifa hadi eneo husika.

Ukweli Muhimu:

- Watu bilioni 3.6 wanaishi bila kuwa na choo salama. ([WHO/UNICEF 2021](#))
- Watu milioni 494 bado wanaenda haja kubwa peupe. ([WHO/UNICEF 2021](#))
- Ukosefu wa takwimu za ubora wa maji kwa zaidi ya watu bilioni 3 unamaanisha kwamba wako katika hatari kwa sababu afya ya maji yao ya chini ya ardhi, mito na maziwa haijulikani. ([UN-Water 2021](#))
- Ulimwenguni kote, angalau watu bilioni 2 hutumia chanzo cha maji ya kunywa kilichochafuliwa na kinyesi. ([WHO 2019](#))
- maji ardhini yanachangia takribani asilimia 99 ya maji yote safi duniani. ([UN-Water 2022](#))
- maji ardhini hutoa nusu ya maji yote yanayotekwa kwa matumizi ya nyumbani, ikiwemo maji ya kunywa kwa idadi kubwa ya wakazi wa vijijini. ([UN-Water 2022](#))
- Kila siku, zaidi ya watoto 800 wenye umri wa chini ya miaka mitano hufa kutokana na kuharisha kunakohusishwa na maji yasiyo salama, usafi na usafi duni wa mwili. ([WHO 2019](#))
- Kila USD1 inayowekezwa katika usafi wa msingi hutokeza hadi USD5 zilizookolewa kwenye gharama za matibabu na kuongezeka kwa tija na kazi hubuniwa kwenye mnyororo mzima wa huduma. ([Hutton et al. 2015](#))

Viunganishi:

#WorldToiletDay

Tovuti ya Siku ya Choo Duniani Mwaka 2022:

www.worldtoiletday.org

Ripoti ya Maendeleo ya Maji ya Umoja wa Mataifa Mwaka 2022:

www.unwater.org/publication_categories/world-water-development-report

Mpango wa Ufuatiliaji wa Pamoja wa WHO/UNICEF wa Usambazaji wa Maji, Usafi na Usafi wa Mwili (JMP):

washdata.org

Ripoti ya UNICEF na WHO ya Hali ya Usafi Ulimwenguni:

www.unicef.org/reports/state-worlds-sanitation

Tovuti-tumizi ya Takwimu ya SDG 6:

www.sdg6data.org

Mfumo wa Kuharakisha SDG 6 Ulimwenguni:

www.unwater.org/publications/the-sdg-6-global-acceleration-framework

Kongamano la Maji la Umoja wa Mataifa Mwaka 2023:
sdgs.un.org/conferences/water2023

Mkutano wa UN-Water Kuhusu Maji Ardhini 2022:
www.groundwater-summit.org

Tovuti ya Umoja wa Mataifa:
www.un.org

Tovuti ya UN-Water:
www.unwater.org